**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**

---

# TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU WIZARA YA MAJI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022; PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

---

**[***Imetolewa chini ya Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020***]**

Mei , 2022

# YALIYOMO

SEHEMU YA KWANZA ........................................................ 1
1.0 MAELEZO YA JUMLA ........................................................ 1
1.1 Utangulizi ........................................................ 1
1.2 Msingi wa Uchambuzi ........................................................ 2
1.3 Mawanda (Scope) ya Taarifa ........................................................ 3
SEHEMU YA PILI ........................................................ 4
2.0 MATOKEO YA UCHAMBUZI NA TATHMINI ........................................................ 4
2.1 Ufafanuzi wa Jumla ........................................................ 4
2.2 Matokeo ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo ........................................................ 5
2.2.1 Ufafanuzi wa Miradi ........................................................ 6
2.2.2 Yatokanayo na Ukaguzi wa Miradi ........................................................ 7
2.2.3 Maoni kutokana na yaliyojitokeza wakati wa ukaguzi wa Miradi ........................................................ 8
2.3 Matokeo ya Uchambuzi wa Taarifa za Mapitio ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 ........................................................ 9
2.3.1 Utekelezaji wa Malengo ya Ukusanyaji wa Maduhuli 10
2.3.2 Utekelezaji wa Majukumu na Mipango ........................................................ 14
2.3.3 Upatikanaji wa Fedha ........................................................ 16
2.4 Matokeo ya Uchambuzi wa Mipango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ........................................................ 17
2.4.1 Mipango na Majukumu kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 ........................................................ 17
2.4.2 Makadirio ya Maduhuli yatakayokusanywa ........................................................ 18
2.4.3 Makadirio ya Matumizi ya Miradi ya Maendeleo ........................................................ 20
2.4.4 Makadirio ya Matumizi ya Kawaida ........................................................ 21
SEHEMU YA TATU ........................................................ 25
3.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI ........................................................ 25
3.1 Maoni ya Kamati ........................................................ 25
3.2 Ushauri wa Kamati ........................................................ 27
SEHEMU YA NNE ........................................................ 30
4.0 HITIMISHO ........................................................ 30
4.1 Maelezo ya Jumla ........................................................ 30
4.2 Shukurani ........................................................ 30

## Orodha

Jedwali Na. 0 1 Mchanganuo wa Mwenendo wa Makusanyo ya Maduhuli...........12
Jedwali Na. 0 2 Mchanganuo wa Upatikanaji wa fedha .....................................16
Jedwali Na. 0 3 Mchanganuo wa Makadirio ya Maduhuli kutokana na Vyanzo vikuu vya mapato ......................................................................19
Jedwali Na. 0 4 Mchanganuo wa Ulinganisho wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 na Mwaka wa Fedha 2022/2023.........................................................................21

# TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA MAJI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

## SEHEMU YA KWANZA

## 1.0 MAELEZO YA JUMLA

### 1.1 Utangulizi

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Maji, kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa hii imegawanyika katika sehemu nne ambazo ni: -

(i) Sehemu ya **Kwanza**: Maelezo ya jumla, inabainisha msingi na muundo wa Taarifa;

(ii) Sehemu ya **Pili**: Ufafanuzi na uchanganuzi, inachambua Matokeo ya Ukaguzi wa miradi ya Maendeleo, Taarifa za Utekelezaji, Upatikanaji wa fedha na uzingatiaji wa Ushauri wa Kamati;

(iii) Sehemu ya **Tatu**: Maoni na Ushauri, inakamilisha uchambuzi kwa kuonesha maoni au mtazamo kutokana na uchambuzi unaojenga msingi wa ushauri wa Kamati; na

(iv) Sehemu ya **Nne**: Inamalizia taarifa kwa kulishauri Bunge kuhusu hoja ya Waziri wa Maji aliyoitoa mapema leo.

## 1.2 Msingi wa Uchambuzi

**Mheshimiwa Spika,** Msingi wa Kamati kuchambua Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Wizara ya Maji ni Masharti ya Kanuni za Bunge. Kifungu cha 6 (7) (a) kikisomwa kwa pamoja na Kifungu cha 7(1)(a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge, kinatambua jukumu la Kamati hii kufanya uchambuzi huo. Aidha, Kanuni ya 117(2) ya Kanuni za Bunge imeweka masharti yaliyotaka Taarifa ya Utekelezaji kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, yachambuliwe na Kamati kabla ya kujadiliwa Bungeni.

**Mheshimiwa Spika**, ili kukidhi masharti hayo, tarehe 30 Machi, 2022, Kamati ilipokea na kujadili Taarifa ya Wizara ya Maji kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023. Katika hatua hiyo, Kamati ilifanya Uchambuzi wa kina na matokeo yake ni Taarifa hii. Kwa msingi huo, ninaliomba Bunge lako Tukufu liipokee taarifa hii na kuijadili sambamba na Hoja ya Waziri wa Maji iliyotolewa mapema leo hii.

## 1.3 Mawanda (Scope) ya Taarifa

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya Utekelezaji na Makadirio ya Mapato na Matumizi yaliyochambuliwa, inagusa maeneo makuu yafuatayo: -

(i) Uzingatiaji wa Ushauri wa Kamati uliotolewa Bungeni wakati wa Kupitisha Bajeti ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022;

(ii) Mapitio ya utekelezaji wa Bajeti ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022;

(iii) Utekelezaji wa kazi zilizofanywa na Wizara ya Maji kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 hadi kufikia mwezi Februari, 2022;

(iv) Kazi zinazopangwa kufanyika kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023; na

(v) Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 MATOKEO YA UCHAMBUZI NA TATHMINI

### 2.1 Ufafanuzi wa Jumla

**Mheshimiwa Spika**, Kanuni ya 117 (1) ya Kanuni za Bunge iliitaka Kamati kutumia siku zisizozidi Saba kwa ajili ya ziara za ukaguzi wa miradi ya maendeleo. Aidha, Kanuni ya 117(2) ya Kanuni za Bunge, ilitoa siku zisizozidi tisa kwa Kamati kufanya uchambuzi wa Taarifa za utekelezaji wa bajeti. Kanuni hiyo inatambua umuhimu wa kufanya ulinganisho kati ya utekelezaji wa bajeti unaoripotiwa na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha unaofuata. Kwa msingi huo, Taarifa hii inaripoti matokeo ya shughuli kuu tatu ambazo ni: -

(a) Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo inayotekelezwa na Wizara ya Maji kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022;

(b) Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022; na

(c) Yatokanayo na uchanganuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

**Mheshimiwa Spika,** Mambo hayo kwa pamoja yameweka msingi wa Maoni na Ushauri wa Kamati. Kwa sababu hiyo, naliomba Bunge lako tukufu lizingatie kwa pamoja matokeo ya Uchambuzi kama unavyofafanuliwa katika Taarifa hii.

## 2.2 Matokeo ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika**, kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, Wizara ya Maji ilitekeleza miradi ya Maendeleo iliyokuwa imetengewa jumla ya Sh. **646,630,000, 000/-**.Wizara ya Maji iliongeza utekelezaji wa miradi ya maendeleo kupitia fedha za Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya UVIKO – 19. Miradi yote kwa pamoja chini ya wizara hii ilipaswa kutekelezwa kwa kutumia jumla ya sh. **785, 983,573,799/=**.

**Mheshimiwa Spika,** msisitizo mkubwa katika utekelezaji ulitarajiwa kuelekezwa kwenye miradi ya kipaumbele kwa maeneo ya mijini na vijijini. Msisitizo maalumu ulihusu pamoja na mambo mengine, usimamizi wa rasilimali za maji, ujenzi na ukarabati wa mabwawa, ubora wa maabara za maji pamoja na kujenga uwezo wa kitaasisi na watumishi. Utekelezaji wa miradi hiyo, ulikusudia kuwawezesha wananchi kupata maji safi, salama na yenye kutosheleza karibu na makazi yao.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilizingatia masharti ya Kanuni za Bunge na kukagua miradi inayotekelezwa na Wizara hii katika mkoa wa Pwani na Dar es salaam. Naomba kulijulisha Bunge matokeo ya ukaguzi wa miradi hiyo kama ifuatavyo: -

### 2.1.1 Ufafanuzi wa Miradi

**Mradi wa majisafi na usafi wa mazingira katika eneo la Kimbiji – Mpera, Jijini Dar es salaam**

**Mheshimiwa Spika**, utekelezaji wa mradi huu unalenga kupunguza tatizo lililokuwa linawakabili wananchi wa Wilaya ya Kigamboni na baadhi ya maeneo ya jiji la Dar es salaam la kukosa uhakika wa maji safi na salama.

Mradi wa majisafi na usafi wa mazingira katika eneo la Kimbiji – Mpera unatekelezwa kwa kutumia vyanzo vya maji vilivyoko chini ya ardhi kwa kuchimba na kuendeleza visima.

Kamati ilijulishwa kuwa Mradi huu unatekelezwa kwa awamu mbili na ulipangwa kukamilika mwezi Aprili, 2022. Hata hivyo, taarifa ilionesha kuwa hadi Kamati ilipotembela Awamu ya Pili ya utekelezaji, ilikuwa imefikia **asilimia 40.**

**Mradi wa Maji Mlandizi – Chalinze**

**Mheshimiwa Spika**, Mradi huu unatekelezwa katika mkoa wa Pwani na unahusu Ujenzi wa Bomba la kusafirisha maji kutoka mitambo ya Ruvu Juu kwenda Mlandizi ukiwa na lengo la kuongeza upatikanaji wa maji kwa kiasi cha **l**ita **9,300,000** kwa siku kwa wananchi wapatao **120,912**.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilijulishwa kuwa pamoja na Mradi huu kukamilika kwa **asilimia 100** wakati Kamati ilipofanya ziara, utekelezaji ulikabiliwa na changamoto kama vile

kuchelewa kwa vibali kutokana na mchakato wa manunuzi na mvua zilizonyesha tofauti na ilivyotarajiwa. Hata hivyo, matokeo ya Mradi huu yameanza kuwanufaisha wananchi wa kawaida na wenye viwanda vinavyochochea ukuaji wa uchumi na ustawi wa watu.

### 2.1.2 Yatokanayo na Ukaguzi wa Miradi

**Mheshimiwa Spika**, Wakati wa ziara za ukaguzi wa miradi inayotekelezwa na Wizara ya Maji, Kamati ilipokea taarifa za utekelezaji wa miradi na kuona hali halisi uwandani (*in the field*) kwa miradi iliyotembelewa. Uchambuzi wa taarifa hizo ulilinganishwa na hali halisi ya hatua zilizofikiwa pamoja na madhumuni ya kutekelezwa kwa miradi inayohusika. Matokeo ya shughuli hiyo yanaonesha kama ifuatavyo: -

(i) Hadi kufikia Mwezi Februari, 2022, fedha za kugharimia utekelezaji wa miradi hiyo zilikuwa zimepatikana kwa kiasi cha **asilimia 76** ya bajeti iliyoidhinishwa na Bunge, ambapo mwenendo wa upatikanaji wa fedha za ndani na fedha za nje ni wa kuridhisha kwani kiasi cha **asilimia 70** ya fedha za ndani zilipatikana na fedha za nje zilizopatikana zilikuwa kiasi cha **asilimia 81** ya makadirio.

(ii) Kwa ujumla hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa miradi iliyopangwa kwa mujibu wa Mpango kazi inatoa matumaini ya kukamilika. Hata hivyo, kwa upande wa Awamu ya Pili ya Mradi wa Kuchimba Visima Eneo la Kigamboni, hatua

ya utekelezaji haina uwezekano wa kukamilika kwa mradi kwa mujibu wa Mpango Kazi.

(iii) Utekelezaji wa miradi umeendelea kwa ushirikiano mkubwa baina ya wananchi na Taasisi zote zinazoshughulikia maji. Ushirikishwaji wa wananchi kwenye miradi inayotekelezwa kwenye maeneo yao, umesaidia kuzuia mkwamo unaoweza kuchelewesha utekelezaji na tija ya mradi.

### 2.1.3 Maoni kutokana na yaliyojitokeza wakati wa ukaguzi wa Miradi

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imezingatia yaliyobainika katika ziara ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo inayotekelezwa na Wizara hii na kupata mtazamo kama ifuatavyo: -

(i) Wananchi ambao ndio wanaufaika na mradi husika wakishirikishwa vizuri katika hatua zote za mradi kuanzia kuibua, kupanga, utekelezaji wa miradi hiyo huendelea vizuri na tija hupatikana. Kwa sababu hiyo, upo umuhimu kwa Serikali kuhakikisha kuwa wananchi wanahusishwa na kushirikishwa inavyostahili katika upangaji na utekelezaji wa miradi ya maji;

(ii) Wananchi wakipata uelewa kuhusu manufaa ya miradi iliyokamilika kwa ajili ya kuwahudumia, huijali na kuitunza miradi hiyo. Hivyo, kuwaelimisha wananchi kuhusu manufaa wanayopata na umuhimu wa kuthamini huduma

endelevu wanayopata, kuchangia na kuimarisha ulinzi wa miundombinu ya huduma za maji; na

(iii) Kwa sababu miradi ya maji inaligharimu Taifa fedha nyingi za walipa kodi, ili miradi hiyo iwe endelevu na ili kuzuia uharibifu wa miundombinu ya maji, ipo haja ya kuwa na ulinzi madhubuti. Kwa msingi huo, Kamati inashauri Serikali ione umuhimu wa kutumia vyombo vya ulinzi na usalama wa raia na mali zao kuhakikisha usalama wa miundombinu ya maji.

## 2.2 Matokeo ya Uchambuzi wa Taarifa za Mapitio ya Utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2021/2022

**Mheshimiwa Spika**, ili kujiridhisha na utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Maji kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, Kamati ilifanya uchambuzi wa mambo makuu matatu ambayo ni:

(i) Uzingatiaji wa Maoni na ushauri uliotolewa Bungeni wakati wa kujadili Makadirio ya Mapato na matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022;

(ii) Ukusanyaji wa Mapato ya Serikali; na

(iii) Utekelezaji wa bajeti ikilinganishwa na upatikanaji wa Fedha.


**Mheshimiwa Spika**, kutokana na uchambuzi huo, naomba kulijulisha Bunge lako tukufu matokeo ya uchambuzi wa Kamati. Lengo ni kuliwezesha Bunge kupata ulinganisho utakaosaidia katika mjadala wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja. Ulinganisho huo unafanyika kwa

kuchanganua kwa njia ya Majedwali ili kurahisisha ulinganifu uliopo. Aidha, chati au grafu zimetumika ili kubainisha taswira ya mlingano uliopo.

### 2.2.1 Utekelezaji wa Malengo ya Ukusanyaji wa Maduhuli

**Mheshimiwa Spika,** Naomba kulikumbusha Bunge lako tukufu kuhusu lengo la Wizara ya Maji la kukusanya maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022. Wakati wa Kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fungu 49, Bunge lilijulishwa kuwa Wizara hii ilikuwa imepanga kukusanya kiasi cha **Shilingi 990,001,000.00.** Vyanzo vikuu vya mapato hayo vinaainishwa katika **Chati Na. 01**.

**Chati Na 0 1 Uchanganuzi wa Maduhuli kulingana na Vyanzo vikuu vya Maji**




**Chanzo:** ***Takwimu zilizotolewa katika Uk. wa 13 wa Randama iliyowasilishwa kwenye Kamati***

**Mheshimiwa Spika,** uchanganuzi unaonesha kuwa Maduhuli ya Wizara ya Maji kwa takriban **asilimia 76** yanatokana na tozo kwa wateja wanaopata huduma za maabara za ubora wa maji zilizopo chini ya wizara hii. Aidha, chanzo kingine kikuu ni malipo ya leseni kwa Kampuni za Utafiti na Uchimbaji wa Visima vya Maji kinachochangia kwenye maduhuli ya wizara kwa karibu **asilimia 24**. Kwa mchanganuo huo, iwapo huduma za maabara zingeboreshwa zaidi na mazingira ya utafiti na uchimbaji visima

vya maji yangevutia zaidi, ukusanyaji wa maduhuli ungeongezeka.

**Mheshimiwa Spika**, ili kujiridhisha na kutimiza wa lengo kuna haja ya kulinganisha lengo na hatua iliyofikiwa katika ukusanyaji. Hadi kufikia mwezi Februari, 2022, maduhuli yalikusanywa kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 01.**

**Jedwali Na. 0 1 Mchanganuo wa Mwenendo wa Makusanyo ya Maduhuli**

| CHANZO | MAKADIRIO YA MADUHULI | MAKUSANYO HALISI HADI MWEZI MACHI, 2022 | ASILIMIA YA LENGO |
|---|---|---|---|
| Mauzo ya Nyaraka | 1,000.00 | 1,800,000.00 | - |
| Leseni za kampuni za utafiti | 240,000,000.00 | 174,902,757.88 | 72.88 |
| Ada - Huduma za maabara | 750,000,000.00 | 380,961,105.00 | 50.79 |
| Jumla | 990,001,000.00 | 557,663,862.88 | 56.33 |

**Chanzo: Takwimu za mwenendo wa makusanyo ya Mahuduli kwenye Randama ya Fungu 49 iliyowasilishwa kwenye Kamati**

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi umeonesha kuwa hadi mwezi Machi, 2022, lengo la jumla la makusanyo ya maduhuli kwa wizara hii lilifikiwa kwa asilimia **56.33** ikiwa ni robo ya tatu ya kipindi cha utekelezaji wa bajeti. Aidha, lengo la ukusanyaji wa maduhuli kutokana na leseni za Kampuni za Utafiti na Ada za

huduma za Maabara ulifikia **asilimia 72.88** na **asilimia 50.79** mtawalia. Mwenendo huo unaonesha mambo yafuatayo: -

(i) Lengo la Wizara katika ukusanyaji wa maduhuli halina dalili ya kufikiwa ifikapo tarehe 30 Juni, 2022. Hali hii inaashiria haja ya kutafakari upangaji wa malengo au usimamizi wa makusanyo ya maduhuli.

(ii) Mwenendo wa Makusanyo kutokana na tozo kwa wateja wanaopata huduma za maabara ya ubora wa maji, hauoneshi matumaini ya kufikia lengo la ukusanyaji. Hali hiyo, ni ishara kwamba, upangaji wa lengo au usimamizi wa ukusanyaji ulikuwa wa mashaka. Hata hivyo, mwenendo huu unaashiria kuwa iwapo huduma za maabara zitaboreshwa zaidi na kusimamiwa ipasavyo, makusanyo ya maduhuli yanaweza kuongezeka.

(iii) Mwenendo wa ukusanyaji wa maduhuli kutokana na malipo kwa ajili ya leseni kwa kampuni za utafiti na uchimbaji wa visima vya maji, unaonesha matumaini ya kufikia lengo la ukusanyaji kutokana na chanzo hicho. Hali hiyo, inaonesha kwamba, upangaji wa lengo au usimamizi wa ukusanyaji ulifanyika kwa uhalisia. Hata hivyo, mwenendo huu unaashiria kuwa iwapo Serikali itafanya uwekezaji, maduhuli yanaweza kuongezeka na kufikia malengo yalikusudiwa.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa uchambuzi huo, Kamati ina maoni kuwa, uboreshaji wa taratibu, masharti na mazingira ya utafiti

na uchimbaji wa visima vya maji inavyostahili, ni suala la kufanyiwa kazi ipasavyo. Aidha, uwekezaji wa kutosha katika huduma za maabara za ubora wa maji utachangia kuongeza mapato ya Serikali na tija ya huduma za maji safi nchini itaongezeka.

### 2.2.2 Utekelezaji wa Majukumu na Mipango

**Mheshimiwa Spika**, Ili kuliwezesha Bunge kusimamia shughuli za Umma katika sekta ya Maji nchini, Kamati ilifuatilia utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Maji yaliyoidhinishwa katika bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

Katika kufanikisha hilo, Moja ya njia iliyotumika ni kufanya mapitio ya hatua iliyofikiwa kwa kazi zilizopangwa kufanyika ndani ya Mwaka wa Fedha 2021/2022 hadi kufikia mwezi Machi, 2022.

Kamati ilidadisi utekelezaji wa majukumu ya wizara katika maeneo makuu matatu ya sekta ya maji. Maeneo hayo ni:-

- Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali za Maji;
- Utoaji wa Huduma za Maji safi na usafi wa mazingira vijijini pamoja; na
- Huduma za Usambazaji Majisafi na Usafi wa Mazingira mijini.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilibaini kuwa shughuli mbalimbali zilizofanyika katika sekta hii zilifanikisha huduma ya maji kwa ujumla na ubora wa maji nchini. Kwa mfano, kuongezeka kwa Maabara za Ubora wa Maji kutoka maabara moja ya Mwanza hadi 17 ni kuongeza uhakika zaidi wa Ubora wa maji. Aidha, kukamilika

kwa jumla ya miradi 305 ikiwemo miradi 265 ya maji vijijini, kunaongeza upatikanaji wa huduma bora za maji safi kwa wananchi.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na mafanikio hayo kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, Ucheleweshaji wa Upatikanaji wa Misamaha ya Kodi unachangia kuchelewa kutekelezwa kwa miradi ya Maji.Kamati ilibaini kuwa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) imepewa siku sitini kushughulikia maombi ya misamaha ya kodi. Utaratibu huo uliowekwa kisheria unaathiri kwa kiasi fulani, utekelezaji wa miradi ya maji. Athari hiyo inachelewesha huduma zinazolengwa kufikiwa katika miradi ya sekta ya maji.

**Mheshimiwa Spika,** Jambo lingine muhimu lililojitokeza ni bajeti ya sekta ya maji ikilinganishwa na mahitaji makubwa ya fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya Maji. Katika hali halisi uwekezaji kwenye huduma za maji kwa hali ilivyo nchini, ni jambo linalohitaji fedha za kutosha zinazopatikana kwa wakati. Kwa taarifa zilizowasilishwa kwenye Kamati, ujenzi wa mabwawa ya kimkakati kama vile bwawa la Kidunda, Farkwa na Ndembera/Lugodwa umechukua muda mrefu kuanza kutekelezwa kutokana na mahitaji makubwa ya fedha kwa wakati mmoja.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ina maoni kwamba, ili ujenzi wa mabwawa ya kimkakati kama bwawa la Kidunda, Ndembera na Farkwa ufikie kukidhi haja ya Huduma za Maji iliyokusudiwa, kuna umuhimu wa kuwa na mkakati maalumu wa kupatikana kwa fedha

kwa ajili hiyo. Vinginevyo, kuna hatari ya kuwa na orodha ndefu ya miradi lakini manufaa yake kwa wananchi yasipatikane kwa wakati.

### 2.2.3 Upatikanaji wa Fedha

**Mheshimiwa Spika**, upatikanaji wa fedha kwa kadiri ilivyopangwa ni jambo linalofanikisha utekelezaji wa Mpango kazi wa shughuli zinazohusika. Aidha, utekelezaji mzuri wa Bajeti unahitaji upatikanaji wa fedha kwa kiasi kilichoidhinishwa na Bunge. Ili kujiridhisha na jambo hilo, uchambuzi wa hali ya upatikanaji wa fedha ulifanyika na uchanganuzi wake unaonekana katika **Jedwali Na. 02**.

**Jedwali Na. 0 2 Mchanganuo wa Upatikanaji wa fedha**

| AINA YA MATUMIZI | BAJETI ILIYOIDHINISHWA | KIASI KILICHOPOKEWA | ASILIMIA |
|---|---|---|---|
| **Mishahara** | 17,742,376,193.00 | 16,964,649,779.00 | **95.6** |
| **Matumizi Mengineyo** | 15,972,209,000.00 | 10,265,165,383.21 | **64.3** |
| **Miradi ya Maendeleo** | 785,983,573,799.00 | 598,529,331,289.40 | **76.2** |
| **JUMLA** | 819,698,158,992.00 | 625,759,146,451.61 | **76.3** |

**Chanzo: Takwimu za Upatikanaji wa fedha kwenye Randama iliyowasilishwa kwa Kamati**

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi umeonesha mwenendo mzuri wa upatikanaji wa fedha ikilinganishwa na kiasi cha bajeti iliyoidhishwa. Hadi kufikia mwezi Machi 2022, Wizara ilikuwa imepokea **asilimia 76.3** ya fedha iliyoidhinishwa.

**Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo.**

Uchambuzi zaidi umebainisha kwamba, wakati Bunge lilipoidhinisha Bajeti ya Wizara ya Maji, bajeti ya miradi ya maendeleo ilikuwa ni **asilimia 95.6** ya Bajeti ya Wizara. Katika Utekelezaji wa Bajeti, fedha zilizopatikana kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ni **asilimia 95.8** ya fedha zote zilizotolewa kwa Wizara ya Maji. Ni maoni ya Kamati kuwa uzito stahiki unaowekwa na Bunge katika Bajeti, ulizingatiwa ipasavyo. Hali hiyo ni jambo la kupongezwa na inastahili kuendelezwa.

## 2.3 Matokeo ya Uchambuzi wa Mipango na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2022/2023

**Mheshimiwa Spika**, Ili kuliwezesha Bunge kujadili Hoja ya Waziri wa Maji kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi, Uchambuzi wa Mipango, Majukumu, ukusanyaji wa maduhuli na makadirio ya Mapato na Matumizi, utasaidia kuonesha mwelekeo. Ili kufanikisha azma hiyo, yafuatayo ni matokeo ya Uchambuzi wa Kamati.

### 2.3.1 Mipango na Majukumu kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa mapitio ya Mpango na Kazi zinazotarajiwa kufanyika ni kigezo muhimu cha kuidhinisha Bajeti, Kamati ilifanya uchambuzi wa kazi hizo. Matokeo ya uchambuzi yanaonesha kuwa usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji, usimamizi wa ubora wa maji, usambazaji wa majisafi mijini na vijijini, pamoja na uimarishaji wa uwezo wa kitaasisi katika sekta ya maji, ni

kazi zinazopewa kipaumbele kwa mfano; mpango wa Wizara unatoa kipaumbele kwa utekelezaji wa miradi ya kimkakati kama vile mabwawa likiwemo Bwawa la Kidunda kwa mwaka wa fedha 2022/2023 mradi huu umeongezewa Bajeti kwa **Shilingi Bilioni 51.5.**

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na hivyo, kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 shughuli zinazoendana na kazi hizo zilikabiliwa na changamoto kama vile kasi ya misamaha ya kodi, upatikanaji wa fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo na upungufu wa wataalamu. Ni maoni ya Kamati kuwa Majukumu yanayopangwa kutekelezwa kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 yanaweza kufanikiwa iwapo changamoto hizo zitatatuliwa.

### 2.3.2 Makadirio ya Maduhuli yatakayokusanywa

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2022/2023, Wizara hii inaomba kuidhinishiwa jumla ya makusanyo ya maduhuli ambayo ni zaidi ya lengo lililowekwa kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022. Uchanganuzi wa hali hiyo unaonekana katika **Jedwali Na. 03**.

**Jedwali Na. 0 3 Mchanganuo wa Makadirio ya Maduhuli kutokana na Vyanzo vikuu vya mapato**

| CHANZO | MAKADIRIO YA MADUHULI 2021/2022 | MAKUSANYO HALISI HADI MWEZI MACHI, 2022 | % LENGO | MAKADIRIO YA MADUHULI 2022/2023 | % ONGEZEKO |
|---|---|---|---|---|---|
| Mauzo ya Nyaraka za zabuni | 1,000.00 | 1,800,000.00 | | 1,000.00 | 0 |
| Leseni za kampuni za utafiti | 240,000,000.00 | 174,902,757.88 | 72.88 | 250,000,000.00 | 4.2 |
| Ada - Huduma za maabara | 750,000,000.00 | 380,961,105.00 | 50.79 | 950,000,000.00 | 26.7 |
| JUMLA | 990,001,000.00 | 557,663,862.88 | 56.33 | 1,200,001,000.00 | 21.2 |

**Chanzo:** ***Takwimu za Upatikanaji wa fedha na Makadirio ya Ukusanyaji wa Maduhuli kwenye Randama iliyowasilishwa kwa Kamati***

**Mheshimiwa Spika**, kwa uchanganuzi huo, matokeo ya uchambuzi yanaonesha ifuatavyo: -

(i) Lengo la ukusanyaji wa Maduhuli kwa Wizara hii limeongezeka kwa **asilimia 21.2**. Jambo muhimu la kuzingatiwa ni kuwa, mwenendo wa ukusanyaji wa maduhuli kwa lengo la mwaka wa fedha unaokwisha haukuonesha urahisi wa kutimia kwa lengo.

(ii) Makadirio ya Mapato kutokana na ada za huduma ya Maabara za ubora wa maji yameongezeka kwa **asilimia 26.7**. Ulinganisho umeonesha kuwa, mwenendo wa ukusanyaji wa ada hizo hadi mwezi Machi 2022 ulikuwa pungufu ya **asilimia 75**. Hali hiyo inaonesha mashaka

iwapo kiasi kinachokadiriwa kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 kinaweza kupatikana.

(iii) Makadirio ya Ukusanyaji wa tozo kwa leseni za Utafiti na Uchimbaji wa visima vya maji, yameongezeka kwa **asilimia 4.2** ikilinganishwa na Mwaka wa Fedha 2021/2022. Uzoefu wa mwenendo wa ukusanyaji wa ada hizo kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 unaonesha uwezekano wa makadirio hayo kuwa na uhalisia.

**Mheshimiwa Spika**, kwa uchambuzi huo, Kamati ina maoni kwamba, lengo la ukusanyaji wa maduhuli lisipozingatia uhalisia, linaweza kupotosha mwelekeo wa maduhuli ya Serikali. Aidha, uwekaji wa malengo ya ukusanyaji wa maduhuli unaweza kuwa na maana katika bajeti iwapo usimamizi wakati wa utekelezaji utakuwa wa uhakika unaozingatia malengo yaliyowekwa.

### 2.3.3 Makadirio ya Matumizi ya Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika**, Wizara hii inaomba jumla ya Shilingi **657,899,338,000/-** kwa ajili ya kugharimia miradi ya maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023. Kiasi hicho ni ongezeko la **asilimia 1.7** ikilinganishwa na kiasi kilichoidhishwa kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 kabla ya kupata fedha za Mpango wa Mapambano dhidi ya UVIKO – 19. Kwa uchambuzi huo, ni wazi kuwa fedha za Mpango wa Mapambano dhidi ya UVIKO – 19 zitaongeza uboreshaji wa huduma za maji safi. Tofauti hiyo inatokana na kukosekana kwa kiasi cha

kufidia shilingi **139,354,573,798.37** zilizopatikana kwa mpango wa kupambana na UVIKO – 19.

### 2.3.4 Makadirio ya Matumizi ya Kawaida

**Mheshimiwa Spika**, uendeshaji wa shughuli za wizara hii hufanyika kwa kutumia fedha za matumizi ya kawaida. Ulinganisho wa uendeshaji wa shughuli za Wizara unaweza kuonekana kwa kulinganisha Makadirio ya Bajeti zinazohusika. Uchambuzi wa Makadirio ya matumizi ya kawaida kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 unaonekana katika **Jedwali Na. 04**.

**Jedwali Na. 0 4 Mchanganuo wa Ulinganisho wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2021/2022 na mwaka 2022/2023**

| AINA YA MATUMIZI | BAJETI ILIYOIDHINISHWA MWAKA 2021/2022 | MAKADIRIO KWA MWAKA 2022/2023 | % ONGEZEKO |
|---|---|---|---|
| **Mishahara** | 17,742,376,193.00 | 34,761,735,000.00 | **95.92** |
| **Matumizi Mengineyo** | 15,972,209,000.00 | 16,700,534,000.00 | **4.56** |
| **JUMLA** | **33,714,585,193.00** | **51,462,269,000.00** | **52.64** |
| | | | |
| **Miradi ya Maendeleo** | 785,983,573,799.00 | 657,899,338,000.00 | **-16.30** |
| **JUMLA** | **819,698,158,992.00** | **709,361,607,000.00** | **-13.46** |

**"**

**anzo:** ***Takwimu za Makadirio ya Matumizi ya Kawaida kwenye Randama iliyowasilishwa kwa Kamati***

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi umeonesha mambo yafuatayo: -

(i) Makadirio ya Bajeti yote ya Wizara ya Maji yamepungua kwa **asilimia 13.46** ikilinganishwa na Bajeti iliyoidhinishwa kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 pamoja na fedha za mapambano dhini ya UVIKO -19;

(ii) Makadirio ya matumizi kwa ajili ya shughuli za uendeshaji yameongezeka kwa **asilimia 4.56** ikilinganishwa na bajeti iliyoidhinishwa kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022;

(iii) Mkadirio ya Matumizi ya shughuli za kawaida yameongezeka kwa **asilimia 52.64**.

**Mheshimiwa Spika**, kwa uchambuzi huo, Kamati imeridhika kwamba Bajeti hii imezingatia azma ya Serikali iliyotamkwa katika ukurasa wa 149 wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020. Azma ni kuona kwamba, nchi inaendelea kuwa na usalama wa maji na kwamba huduma ya maji safi na salama inaendelea kuimarishwa. Makadirio ya matumizi ya kawaida kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 yanaakisi lengo hilo. Muhimu kwa Serikali ni kuhakikisha kuwa Bajeti inayoidhinishwa na Bunge inatekelezwa ipasavyo.

### 2.3.5 Ulinganisho wa Uwiano wa Bajeti ya Maendeleo na Makadirio ya Jumla

**Mheshimiwa Spika**, Miradi ya Maendeleo katika Sekta ya Maji inahusika na kuboresha huduma za maji, upatikanaji wa maji safi na uendelezaji wa rasilimali za maji nchini. Uwiano wa Bajeti ya Miradi hiyo na Bajeti ya uendeshaji unasaidia kupata taswira ya hatua za Serikali kuboresha huduma na maisha ya wananchi. Kwa msingi huo, ulinganisho wa uwiano kati ya Bajeti ya maendeleo na jumla ya makadirio ya matumizi ulifanyika kupata taswira hiyo. Naomba kulijulisha Bunge kuwa Kamati imebaini yafuatayo: -

(i) **Asilimia 92.7** ya bajeti ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 ni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Lakini kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 **Asilimia 95.8** ya bajeti pamoja na fedha za UVIKO ilikuwa ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

(ii) Fedha ya Matumizi ya kawaida imeongezeka na kufikia **Asilimia 7.3**, hali hiyo inaonesha kuwa kuna msisitizo mkubwa kwenye miradi ya maji na usafi wa mazingira jambo linalotoa matumaini ya kuboresha maisha ya wananchi;

(iii) Kwa upande wa Bajeti Kuu **Asilima 37.79** inategemewa kuwa makadirio ya bajeti ya maendeleo. Uwiano huu ukilinganishwa na uwiano kwenye bajeti ya Wizara ya Maji, inaonekana wazi kwamba Serikali imedhamiria kuendeleza huduma na miundombinu ya maji safi na usafi wa mazingira.

**Mheshimiwa Spika**, kwa uchambuzi huo, Kamati inaipongeza Serikali kwa mtazamo huo wa kimaendeleo katika sekta ya maji nchini. Uwiano wa bajeti uliochanganuliwa ni ishara ya hatua za kutimiza lengo la huduma ya majisafi na salama kwa kuwafikia wakazi asilimia 85 kwa vijijini na asilima 95 kwa mijini ifikapo mwaka 2025. Kikubwa cha kusisitiza ni kuendelea kuiwezesha sekta hii kupata fedha kadiri inavyoidhinishwa na Bunge.

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

### 3.1 Maoni ya Kamati

**Mheshimiwa Spika,** Maoni ya Kamati yanatokana na majadiliano ya kina kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023. Maoni haya ambayo ni egemeo la Ushauri wa Kamati yanazingatia changamoto zinazoikabili sekta ya maji ambazo ni pamoja na upatikanaji wa fedha za kutosha na kwa wakati, upungufu wa vyanzo vya maji unaotokana na shughuli za binadamu, mabadiliko ya tabianchi, uharibifu wa mazingira, upotevu wa maji mijini na ongezeko la idadi ya watu.

**Mheshimiwa Spika,** kwa msingi huo, maoni au mtazamo wa Kamati ni kama ifuatavyo: -

(i) Kazi nzuri inayofanywa na Wizara ya Maji katika kufanikisha azma ya kuwezesha usalama wa maji na kuimarisha huduma ya maji safi na salama, pamoja na usafi wa mazingira kama ilivyoahidiwa katika Ilani ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020 inastahili pongezi;

(ii) Mipango mizuri ya kuendeleza miradi ya kimkakati ikiwemo kuanza utekelezaji wa bwawa la Kidunda, ni utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi na Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa 2021/2022 – 2025/2026. Kwa sababu hiyo hatua hii inafaa kupongezwa na kusisitizwa ili iendelee kwa mabwawa mengine ya Farkwa na Ndembera;

(iii) Uelewa wa kutosha na stadi za msingi kuhusu utatuzi wa kero za wananchi ni mambo muhimu kwa Watumishi wa Sekta ya Maji ili kufanikisha lengo la huduma za maji safi na salama kufikia **asilimia 85** ya wakazi wa vijijini na **asilimia 95** ya wakazi wa mijini. Takwimu zinaonyesha upatikanaji wa maji kwa umefikia **asilimia 74.05** kwa wakazi wa vijijini na **asilimia 86.5** kwa wakazi wa mijini;

(iv) Mikakati ya kuvuna maji ya mvua inaweza kuongeza upatikanaji wa majisafi na salama. Hata hivyo, pasipo kutoa elimu na hamasa kuhusu jambo hilo, faida ya maji hayo inaweza kukosekana wakati wa kiangazi ambapo hakuna mvua;

(v) Kutotafuta ufumbuzi wa Changamoto ya upatikanaji wa vibali vya ununuzi wa vifaa vinavyohitajika kwenye mradi (*Government Notice*) ni sawa na kuendelea kukumbatia vikwazo vya kutekeleza miradi ya maendeleo katika sekta ya maji. Hali hiyo, inaathiri juhudi za kuimarisha utoaji wa huduma za majisafi na usafi wa mazingira;

(vi) Kukosekana kwa huduma ya maji safi ya uhakika katika jiji la Dodoma ambalo ni makao Makuu ya Nchi, ni jambo linalohitaji mkakati mahsusi na nia thabiti kulitatua. Aidha, uwezekano wa kutumia maji kutoka ziwa victoria kwa ajili ya huduma ya maji safi kwa mkoa wa Dodoma usipotekelezwa, itakuwa ni vigumu kumaliza changamoto ya upatikanaji wa maji ya uhakika kwa wakazi wa Dodoma.

(vii) Ujenzi wa Miundombinu ya majitaka katika Miji na Makao Makuu ya Mikoa unaweza kusaidia usafi wa miji na kuzuia milipuko ya magonjwa yanayosababishwa na kutozingatiwa kwa usafi;

(viii) Ujenzi wa mabomba makubwa ya kusambazia maji vijijini usipozingatia kuwapatia maji wakazi wa vijiji vinavyopitiwa na mabomba hayo, unakosa msingi wa haki ya kupata huduma hiyo kwa wakazi wa vijiji hivyo; na

(ix) Kutokutumia mfumo wa malipo kabla ya matumizi (*postpaid*) ni miongoni mwa sababu za kuwepo kwa kero ya ankara za maji kwa wananchi.

## 3.2 Ushauri wa Kamati

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na maoni yaliyobainishwa hapo juu sasa naomba kutoa ushauri ufuatao: -

(i) Serikali iendelee kuhakikisha kwamba fedha zinazoidhinisha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya Maendeleo ya kimkakati zinapatikana inavyostahili;

(ii) Serikali iongeze juhudi za kuwaelimisha wananchi kutumia utaratibu wa kuvuna maji ya mvua wakati wa majira ya mvua ili yasaidie wakati wa kiangazi. Aidha, kwa kuwa utekelezaji wa jambo hili umekuwa ni wa kusuasua kwa muda mrefu, kwa ajili ya utekelezaji bora na kuwekewa mkazo ni vyema tukawa na sheria ya uvunaji maji;

(iii) Serikali itafute suluhisho kwa changamoto ya upatikanaji wa vibali vya ununuzi wa vifaa vya maji (*Government Notice*) ili kufanikisha utekelezaji wa miradi hiyo kwa wakati;

(iv) Serikali iendelee kutekelezaji kwa kasi mipango ya ujenzi wa miundombinu ya majitaka katika miji na makao makuu na mikoa ili kuzuia na kuondoa milipuko ya magonjwa kutokana na majitaka;

(v) Serikali iharakishe Utekelezaji wa Mpango wa kutoa maji Ziwa Victoria kwa ajili ya kutatua changamoto ya upatikanaji safi safi na salama katika Jiji la Dodoma na viunga vyake;

(vi) Wizara iweke utaratibu kwa Mamalaka za Maji za Mikoa ambazo ni changa kubadilishana uzoefu juu ya uboreshaji wa huduma za maji safi na usafi wa mazingira kwa Mamlaka za Maji zenye uzoefu na ambazo zimefanikiwa kwenye utekelezaji wa miradi ya maji;

(vii) Wizara ya maji iharakishe utekelezaji wa mfumo wa malipo kabla ya matumizi (*postpaid*) ili kukabiliana na kero inayowakuta wananchi kutokana na kuongezewa madai ya maji katika Ankara zao;

(viii) Wizara iimarishe utoaji wa takwimu sahihi za upatikanaji wa huduma ya maji safi kwa wakazi wa vijijini na mijini kwa sababu ukosefu wa takwimu sahihi unakwamisha mipango ya ya upatikanaji maji na ni vigumu kupima mafanikio yaliyofikiwa kulingana na malengo yaliyowekwa; na

(ix) Ujenzi wa mabomba kwa ajili ya usambazaji na upatikanaji wa maji vijijini uzingatie umuhimu wa vijiji vinavyopitiwa na

mabomba hayo kupata huduma ya maji. Aidha, ili kulinda miundombinu ya maji ni muhimu kwa miradi ya maji vijijini kuwa na mabirika kwa ajili ya wafugaji kunyweshea mifugo;

## SEHEMU YA NNE

## 4.0 HITIMISHO

### 4.1 Maelezo ya Jumla

**Mheshimiwa Spika**, jukumu la Kamati katika Hoja ya Waziri wa Maji kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ni kuchambua makadirio hayo na kulinganisha na taarifa za utekelezaji wa majukumu ya wizara hiyo kwa mwaka wa fedha unaoisha. Baada ya kutekeleza hayo, nimeisoma Taarifa hii kwa kuonesha matokeo ya Uchambuzi, Maoni kutokana na matokeo hayo pamoja na kubainisha ushauri kwa msingi wa maoni ya Kamati.

### 4.2 Shukrani

**Mheshimiwa Spika**, kwa niaba ya Kamati napenda kukupongeza wewe binafsi na Naibu Spika kwa namna mnavyotekeleza majukumu yenu kwa umakini na weledi wa hali ya juu ambayo vimeliwezesha Bunge kutekeleza wajibu wake wa kuisimamia na kuishauri Serikali kwa ustadi wa hali ya juu.

**Mheshimiwa Spika**, napenda pia kumpongeza na kumshukuru Waziri wa Maji Mhe.Juma Aweso, (Mb) na Naibu Waziri Mhe. Mhandisi Maryprisca Mahundi (Mb), Katibu Mkuu – Mhandisi Anthony Sanga na Naibu Katibu Mkuu Mhandisi Nadhifa Kemikimba pamoja na Wataalamu wa Wizara ya Maji kwa ushirikiano waliotupatia Kamati wakati wa kuchambua na kujadili Bajeti ya Wizara.

Aidha, nawashukuru kwa moyo wa dhati wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano wao wa namna ambavyo wamejitoa kikamilifu katika

utekelezaji wa majukumu ya Kamati ya kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji. Wajumbe walijitoa kikamilifu na kutekeleza majukumu ya uchambuzi kwa moyo na weledi wa hali ya juu. Hali hiyo ni ushahidi tosha kwamba, Wajumbe wa Kamati hii wako tayari kulitumikia Bunge, Taifa na wananchi wakati wowote.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kutambua na kuthamini umuhimu wa Wajumbe wa Kamati ningetamani kuwatambua kwa kuwataja majina yao. Hata hivyo, kwa kuzingatia ufinyu wa muda naomba majina yao yaingizwe kwenye kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge (*Hansard*). Majina ya Wajumbe hao ni haya yafuatayo: -

1. Mhe. Dkt Christina Gabriel Ishegoma, Mb Mwenyekiti
2. Mhe. Athuman Almas Maige, Mb
3. Mhe. Job Yustino Ndugai, Mb
4. Mhe. Balozi Dkt Bashiru Ally Kakurwa Mb
5. Mhe. Prof.Sospeter Mwijarubi Muhongo, Mb
6. Mhe. Deo Kasenyenda Sanga, Mb
7. Mhe. Charles John Mwijage, Mb
8. Mhe. Christopher Olonyokie Ole Sendeka, Mb
9. Mhe. Livingstone Joseph Lusinde, Mb
10. Mhe. Munde Tambwe Abdallah, Mb

11. Mhe. Janejelly James Ntate, Mb
12. Mhe. Anna Richard Lupembe, Mb
13. Mhe. Khadija Hassan Aboud, Mb
14. Mhe. Dkt. Rita Enespher Kabati, Mb
15. Mhe. Kunti Yusuph Majala, Mb
16. Mhe. Prof Patrick Alois Ndakidemi, Mb
17. Mhe. Mohamed Suleiman Omar, Mb
18. Mhe. Furaha Ntengo Matondo, Mb
19. Mhe. Benaya Liuka Kapinga, Mb
20. Mhe.Jackson Gedion Kiswaga, Mb
21. Mhe Tumaini Bryceson Magessa, Mb
22. Mhe Mrisho Mashaka Gambo, Mb
23. Mhe. Michael Mwita Kembaki, Mb
24. Mhe. Yahya Ali Khamis, Mb
25. Mhe. Yustina Arcadius Rahhi, Mb
26. Mhe. Prof. Shukrani Elisha Manya, Mb
27. Mhe. Emmanuel Peter Cherehani, Mb

**Mheshimiwa Spika**, mwisho napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Nenelwa Mwihambi, Mkurugenzi wa Idara ya Kamati Ndg. Athuman Hussein, Kaimu Mkurugenzi Msaidizi Sehemu ya Kamati za Fedha Ndg. Dickson Bisile pamoja na Makatibu wa Kamati Ndg. Rachel Nyega na Ndg. Eunike Donati Shirima wakisaidiwa na Ndg. Waziri Kizingiti kwa kuihudumia Kamati na kukamilisha taarifa hii kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji, kwa nwaka wa fedha 2022/2023 kama yliyowasilishwa na mtoa hoja hapo awali.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

Dkt. Christine Gabriel Ishegoma, Mb

**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI**

12 MEI, 2022